


# UPENDO WA KIUNGU

 . . .tukiondoka tu mkutanoni, na tukaenda kumwona mwanamke, rafiki yetu, Bibi Dobleman, huko Edmonton, Alberta. Nasi tulikuwa tu maili ishirini hivi kutoka mpakani mwa Canada, tulipopata habari ya kwamba ndugu yangu alikuwa yuafa. Kwa hiyo tukageuka moja kwa moja, kupitia dhoruba ya theluji, nasi tukaanza kurudi moja kwa moja nyumbani, tukisafiri kwa siku kumi na moja. Nasi tulifika jana jioni sana, na kuamka tumechelewa jana usiku, halafu mapema tena asubuhi ya leo, nimechoka sana.

<sup>2</sup> Lakini mara nilipofika kwa mama yangu, baada ya kupata mahali ambapo tungepiga simu tena, yeye akasema, “Ndugu Neville amekuwa huko nje.” Huyu ni mchungaji halisi, jamani. Hiyo ni baadhi ya . . . Hakika tunathamini hilo. Sasa, huenda isininii . . . Labda, wapendwa wenu kamwe hawajafikia mahali hapo, labda. Lakini katika saa ya upeo wa hatari, unapojua kwamba jambo fulani linatukia, na kujua ya kwamba rafiki yako atashikana nawe. Basi nikakimbia kwa ndugu yangu.

<sup>3</sup> Basi nilipoenda, mara nilipoingia, nilibadilisha tu nguo na kukimbia kule. Nilimkuta nani chumbani, katika maombi, ila Ndugu Neville; chumbani mle pamoja na Howard, katika maombi.

<sup>4</sup> Ni—ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Na—nami ni afadhali niseme papa hapa jukwaani, kama nilivyosema sikuzote, “Afadhali nikupe tumba dogo la waridi sasa, kuliko shada zima ukiisha kutuacha.” Sasa hivi ndio wakati wa kufanya hilo.

<sup>5</sup> Nami ninamthamini Ndugu Neville. Nami najua sote tunamthamini, humu kanisani, kwa kuwa mchungaji shujaa. Kumwonyesha tu jinsi mnavyomthamini, inueni mikono yenu namna *hii*, kwa Mungu. Jambo ndilo hilo. Asanteni. Hilo kweli ni jambo ambalo . . .

<sup>6</sup> Nilienda nyumbani; nikamwambia mke wangu. Nikasema, “Mpenzi, nilipoenda nikabisha mlangoni . . . Niliponyoka ukumbini, nikasoma chati, nione hasa nini kilikuwa kibaya. Basi nikashuka kule chini, nami nikasikia kitu fulani mle ndani. Ndipo nikagonga kidogo mlangoni. Nilidhani ilikuwa ni mtu akinena. Alikuwa amemketisha kitandani pamoja na Biblia yake, huku wote wawili wameinamisha vichwa vyao, wakimwomba Mungu, nilipoingia. Nisingefanya chochote ila kuungana nao katika maombi.”

<sup>7</sup> Na—na, pia, maombi yangu, kumwambia Mungu ya kwamba ninamthamini rafiki halisi na mchungaji halisi. Na hebu Ndugu Neville na aishi muda mrefu katika ulimwengu huu, ku—

kumtumikia Bwana. Ninaamini Mungu amemweka hapa kwa miaka mingi, mingi sana, kumtumikia, mtu ambaye ni shujaa. Iliugusa moyo wangu kwa kilindi zaidi ya vile nimekuwa kwa muda mrefu.

<sup>8</sup> Sasa, kwa kawaida, sasa, kwamba. . . Darasa la shule ya Jumapili halijaruhusiwa kuondoka bado, kurudi katika—katika watoto. Kwa hiyo nilifikiri kwamba, labda, huenda ikawa tutawaombea wagonjwa. Sikufanya matangazo yoyote ya kuja humu, kuwaombea wagonjwa. Lakini ikiwa kuna yeyote hapa wa kuombewa, basi tutawaombea tu.

<sup>9</sup> Sasa, kama Dada Gertie, kama atapanda huku, atuchezee *Ni Tabibu Wa Karibu*. Nasi tutamwomba Baba yetu mpendwa wa Mbinguni, kama atawabariki wale wanaomhitaji leo. Halafu tunataka kuninii, wote walio wagonjwa na wahitaji, wakusanyike tu hapa madhabahuni.

<sup>10</sup> Sijakosea, huyu ni Nellie Sanders anayekuja hapa? Jamani! Mungu akubariki, Nellie. Miaka ishirini na mitano, imekuwa. Mungu akubariki, Nellie. Niliangalia huku, muda mfupi uliopita, nikakuangalia. Nami sikutaka ufikirie. . . kuangalia, kumkodolea mtu macho. Niliendelea kuangalia nyuma, nami nikawazia ilionekana kama ni Nellie.

<sup>11</sup> Hakuna mmoja wenu hapa labda anayekumbuka. Nadhani baadhi yenu. . . Ni wangapi wanaomkumbuka Nellie Sanders? Vema, bila shaka. Naye alikuwa ni mmoja wa waliokuja kwanza maskanini. Yeye na mke wangu aliyetuacha walikuwa ni marafiki wasiri na dada, katika Kristo. Nao. . . Yeye aliolewa hapa, mmoja wa Wenye Kujitolea Marekani, afisa katika huduma hii. Naye, ndugu yetu, ameenda kuwa pamoja na Mungu. Akamwacha, nafikiri, akiwa na wavulana wawili, nafikiri; watoto kadhaa, kwa vyovyote vile, baadhi yao wangali shuleni. Naye Nellie anazunguka—zunguka peke yake, na kuingia tu katika umri wa wasiwasi sana na kuvurugika. Alinipigia simu nilipokuwa Phoenix, Arizona, mkutanoni, kwa ajili ya maombi. Mambo mengi yanarudi, Nellie, kwenye wakati unga wa mbaio sakafuni, nawe pamoja na Hope, yule msichana wa Adcock, na wengi wao walipokuwa hapa. Hiyo ni miaka mingi iliyopita, miaka ishirini na mitano iliyopita. Kupitia tu karibu nami. Tu—tunashuka barabarani, upesi sana, hiyo ni kweli.

<sup>12</sup> Vema, Mungu awe pamoja nawe sasa. Wale walio wagonjwa na wanataka kupanda huku madhabahuni kwa ajili ya maombi, mimi na mchungaji wetu tutaungana pamoja katika maombi kwa ajili yenu. Njoni moja kwa moja.

<sup>13</sup> Halafu, kidogo, mara baada ya haya, ujumbe mfupi kwa ajili yenu tu, wa ibada ya kuhubiri. Laiti ungaliweza kukaa. Tutamalizia na ibada ya shule ya Jumapili, baada ya maombi kwa ajili ya wagonjwa. Ndipo tutaingia moja kwa moja kwenye ibada nyingine, nami nina matangazo machache nitakayofanya.

Tabibu huyu mkuu sasa yuko karibu,  
 Yesu mwenye huruma;  
 Anaunenea moyo uliohuzunika ukafurahi,  
 Hakuna Jina jingine ila Yesu.

<sup>14</sup> Sasa, kama tungeweza tu kuingia katika ushirika wa maombi haya, uponyaji kwa kila mmoja, tukijua ya kwamba Mungu yuko hapa, naye aliahidi kujibu.

<sup>15</sup> [Ndugu Neville anasema, “Dada mmoja angetaka kuombewa.”—Mh.] Naam, hiyo ni sawa, tutashuka tukamwombe, yule mama aliyeketi chini. Bila shaka. Vema, Ndugu Neville, waweza kuja, kusaidia?

<sup>16</sup> Sasa, kama mtakuwa tu na kicho iwezekanavyo, hawa jamaa wadogo wanachukua viti vyao. Basi na tuombe sasa, ili tutakaposhuka kuwapaka mafuta wagonjwa na wanaoteseka, tutamwamini Mungu, kuamini. Tuamini kwamba Mungu atayatimiza.

<sup>17</sup> Ninyi nyote huko nje kwenye wasikilizaji, mlio wazima, asubuhi ya leo, msiohitaji kuja madhabahuni, wazienu tu sasa, ya kwamba, neema ya Mungu ndiyo iliyowaleta hapa. Sasa ninyi waombeeni hawa wengine walio madhabahuni hapa, vijana kwa wazee.

<sup>18</sup> Kama desturi yao hapa maskanini, tunamtuma mchungaji, kupaka mafuta. Tunawaomba. Kisha tutamtuma mchungaji, kuwapaka mafuta. Ninaambatana naye, kuwawekea wagonjwa mikono, wakati akiwapaka mafuta. Maandiko, “Wapakeni wagonjwa mafuta, katika Jina la Bwana. Wawekeeni mikono, nao watapona.” Maandiko!

<sup>19</sup> Sasa, ninyi nyote, pamoja, mnapoviinamisha vichwa vyenu sasa, wakati tukiomba pamoja kwa ajili ya wagonjwa.

<sup>20</sup> Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja kwenye Uwepo Wako wa Kiungu kwa unyenyekevu sasa, kwa njia ya wahitaji, wagonjwa, wale wasioweza kujisaidia. Na wengi wao, Baba, wamepita usaidizi wa daktari. Hakuna kinachoweza kufanywa isipokuwa wapewe neema Yako. Ninaomba, kwa unyenyekevu, leo hii, Mungu, kwa moyo wangu wote, nikiungana na kanisa hili dogo, ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu, ambaye yupo sasa, kulithibitisha Neno la Bwana Yesu aliyesema, “Popote walipo wawili au watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao. Wakiomba lolote, linalohusu kitu chochote, watalipokea.” Hilo ni Neno Lako la Milele, Bwana, lililonenwa hata kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, limetolewa kwetu na Nabii, na Mwana wa Mungu, Mwenyewe.

<sup>21</sup> Sasa, shauku yetu kuu sasa, Baba, ni Wewe uwaponye wagonjwa, wahitaji walio hapa madhabahuni. Ninaomba ya kwamba utampa tu kila mmoja baraka maalum ya imani sasa hivi. Kwamba, tunapoenda, mimi pamoja na mtumishi Wako, kutia mafuta na kuweka mikono juu ya hawa watu, jalia Roho

Mtakatifu anyoshe ndani kwa kilindi, pamoja na imani moyoni mwangu, na jalia kila mmoja aponywe. Tunaomba katika Jina la Kristo, kwa ajili Yake.

<sup>22</sup> Sasa huku mumeinamisha vichwa vyenu, kila mtu akiwa katika maombi, mimi pamoja na mchungaji tunaenda kuomba. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Mbingu na nchi zinakusifu Wewe,  
Mbingu na nchi zinakusifu Wewe,  
Ee Bwana Uliye Juu Sana.

<sup>23</sup> Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya somo la shule ya Jumapili, jinsi ambavyo limeichochea mioyo yetu. Jalia tujitayarisha asubuhi ya leo, na tutoke kwenye vifungo vya kutokuamini, tuwe huru tunapotembea. Tunajua Malaika wa Bwana ataenda mbele zetu, akilithibitisha Neno la Mungu, na kumweka huru kila mmoja wetu kutoka kwenye vifungo vya hofu, na maradhi, na dhiki, na ugonjwa, na mateso, kwa kuwa Mungu ameahidi kufanya hivyo. Kila mtu aliyefungiwa kwenye hali kama hizo, asubuhi ya leo, jalia Nuru ya Mungu iangaze juu yao, siku ii hii tu. Na jalia waondoke hapa, wakiwa wazima. Asante kwa ajili ya Ujumbe na kwa ajili ya Neno Lako, kwa uongozi wa Roho Mtakatifu. Tujalie baraka hizi, Baba. Na sasa kuwa pamoja nasi katika ibada ya mahubiri ya asubuhi ya leo, kwa ajili ya maskini Ujumbe mfupi, unaokuja. Tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

<sup>24</sup> Sasa, kwa dakika chache tu, wale ambao inabidi waondoke sasa, hebu tusimame tu tunapoimba wimbo. Inga-... *Peleka Jina La Yesu*. Wale ambao inabidi waondoke wanaweza kuruhusiwa kwenda. Wale wanaoweza kubaki kwa dakika zingine thelathini, tungefurahia mkibaki. Vema.

Peleka Jina la Yesu,  
Mtoto wa huzuni na . . .

Geuka moja kwa moja ukapeane mikono na mtu fulani karibu nawe.

. . . litakupa furaha na faraja,  
Peleka kila uendako.

Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo ni tamu  
jinsi gani! (Loo ni tamu jinsi gani!)  
Tumaini la duniani na furaha . . . (. . . ? . . . )  
. . . na . . .

<sup>25</sup> Amina. Ketini. Na Bwana awabariki ninyi nyote, sana, vema. Ndio kwanza nione, tuna baadhi ya *Mbiu za Imani* hapa, ile programu ndogo, gazeti dogo la Ndugu Joseph Boze huko Chicago, ndugu mzuri sana. Sikuzote sisi . . . Tumekuwa na ushirika mkuu sana, mmoja na mwingine. Tunao wakati mzuri kila wakati tunapoenda Chicago. Pamoja naye tu, siku chache

zilizopita usiku, tena. Nayo ni bure. Njoo tu, ujichukulie moja, baada ya ibada kwisha. Yako hapa chini.

<sup>26</sup> Sasa, tuna furaha kuwaona wengi wenu mngali mumemshikilia Kristo. Na sasa, kwa dakika chache tu za muda wenu, ningetaka kunena jambo fulani, kwa sababu ya kuwa hapa pamoja nanyi.

<sup>27</sup> Nimechoka. Sauti yangu iko chini. Nami nilikuwa na mikutano mikubwa. Huko Indianapolis, ulikuwa ni mkutano mkubwa, mzito. Nao usiku huo tulikuwa na furaha sana kuona mamia wakishuka kwenye maskani hiyo, yapata watu elfu kumi wameketi, wakishuka kuja kuitoa mioyo yao kwa Kristo, usiku huo.

<sup>28</sup> Naye Russell Ford na hao wengine, jinsi walivyochangamshwa. Na—na kazi ya huyo Cadle, Ndugu Cadle alianza miaka mingi iliyopita, angali anaendelea. Mnajua, ningependa kuwa na mahali kama hapo, siku moja. Ni moja ya mahali pakuu sana nilipopata kuona, jinsi tu palivyojengwa. Na kuna kitu fulani tu kuwahusu, huko. Nafikiri mimi ni mwepesi kushikwa na hisia. Ninapooona kazi kuu ambayo mtu fulani ameanza, ninashikwa na hisia kwa ajili ya hiyo.

<sup>29</sup> Sasa, kwa kuwa nimepwelewa na sauti, nasi tumekuwa huko juu mlimani, tukijaribu kumfikia mwanamke mgonjwa, rafiki yetu, huko juu Canada. Tulikuwa karibu kuvuka mpaka, niliposikia habari kwamba ndugu yangu alikuwa yuafa, ndipo nikarudi. Nasi tukaendesha gari siku baada ya siku, na usiku baada ya usiku, tumeketi siku kumi kwenye gari hilo. Kwa hiyo mnaweza kuwazia jinsi ninavyojisikia asubuhi ya leo.

<sup>30</sup> Na, lakini, ninawashukuru ninyi nyote, tena, kwa kumwomba ndugu yangu, maana yeye, inaonekana kama, yuko njiani kupona tena. Mungu amempa nafasi nyingine. Na kwa hiyo na—nawashukuru, nami ninamsifu Mungu kwa ajili ya mambo yote.

<sup>31</sup> Maamuzi mengi makubwa ya kufanya bado. Safari ya ulimwenguni kote inakuja. Afrika inanimulikia usoni. Na mahali pengi kila mahali, hata sijui nigeukie wapi, kila mahali, kila mahali. Na kuna yapata, angalau makongamano kumi ama zaidi, makubwa, muhimu sana yaliyowekwa sasa hivi, na kila moja likituita twende. Sina budi kufanya namna fulani ya uamuzi, katika saa ishirini na nne zijazo, kwa ajili ya hatua inayofuata. Kwa hiyo, niombeeni. Niombeeni. Nami na—nahitaji maombi yenu.

<sup>32</sup> Ninatumaini, kufunga kipepeo hicho, hakikuwasumbua ninyi nyote hapa mbele kupita kiasi, kwa dakika moja.

<sup>33</sup> Ni—nimeona mambo mengi sana maishani mwangu, ya kusafiri kwa ajili ya Bwana, katika hali za kila namna na magonjwa na—na ukoma. Pia nimewakumbatia wenye ukoma, nikawapa mikono, na—na kila aina ya ugonjwa. Na

nikaingia kwenye wadi na kambi zao za kutenga wagonjwa wa kuambukiza, na kila kitu, kote ulimwenguni, karibu kote.

<sup>34</sup> Wala mimi—mimi—mimi si mvulana tena. Nellie, nadhani unajua hivyo. Nami ninaelekea kwenye umri wa...Ndipo ninamsikia Ndugu Bosworth, hivi majuzi huko juu, karibu na umri wa miaka tisini. Naye, nilipokuwa Indianapolis, alikuwa na donge la damu lililoingia moyoni mwake. Alikuwa na mapambano ya kifo kooni mwake, amepoteza fahamu. Bibi Bosworth akanipigia simu nimwombe.

<sup>35</sup> Nikaenda huko, nasi tukalitangaza na kuingia katika maombi. Kesho yake, akanipigia simu, kasema, “Ningetaka kuwa mkutanoni pamoja nawe, siku moja.” Halafu mimi ninajisikia namna hiyo hapa, kwenye umri wa miaka arobaini na saba, ninapaswa kujionea aibu. Lakini ninii tu—lakini ni sehemu ya mwanadamu tu, nadhani.

<sup>36</sup> Lakini, loo, jinsi lilivyo la thamani, na ni la ajabu jinsi gani! Hakuna kinacholingana na kuokoka! Kuokoka! Hata, hutambui, ewe rafiki, nina hakika, ya kwamba ibilisi hukuficha hilo kadiri awezavyo, (anafanya hivyo kwangu), kutambua kile thamani ya nafsi ilicho. Je, mlipata kuwazia tu kile ilicho, na kile Umilele unachomaanisha, na kwamba utakuwa hivyo kwa muda gani? Unaona? Unatambua, huu ndio wakati ambapo unafanya uamuzi wako kwa ajili ya Umilele.

<sup>37</sup> Jumapili iliyopita, nikiwa pamoja nanyi hapa, ninaamini nilihubiri juu ya hakikisho, zile nguvu ambazo Mungu alikuwa ameahidi; na kuwachagua na kuwaita kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na kuandika jina lako katika Kitabu Chake. Hukuwa na uhusiano wowote nalo. Mungu alifanya hivyo. Si ni ajabu hiyo? Mwana-Kondoo alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wala (kwa nini?) halikutukia mpaka miaka elfu nne baadaye. Lakini, Mungu, wakati alipolinena, ilimbidi kulifanya, maana Yeye hana budi kulitimiza Neno Lake. Basi wakati ule ule ambapo Mwana-Kondoo aliandikwa, ninii lako...uliandikwa pamoja Naye. “Majina yetu yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo,” sio usiku ule tuliomjia Kristo, bali, “kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,” Biblia ilisema. Kwa hiyo hilo ndilo hakikisho. Naye ndugu aligusia hilo asubuhi ya leo katika kusoma huku kuzuri sana kwa shule ya Jumapili.

<sup>38</sup> Sasa hebu tusome tu Andiko mahali fulani, kwa ninii kidogo tu...ninataka...jambo fulani tu lililo moyoni mwangu. Ningetaka tu kulizungumzia kwa dakika chache, kisha tutafumukana. Na kutarajia ibada tena usiku wa leo. Na sasa, nilipata ujumbe moyoni mwangu, nikishuka huku hivi majuzi, nami nataka, Mungu akipenda, kama nitakuwa nimerudi hapa Jumapili ijayo asubuhi, kuuleta maskanini kwanza. Jambo fulani tu lililo moyoni mwangu, la wakati huu.

39 Nilienda mahali fulani kula. Nami nikawazia, “Vema, kwani ninaingia kichaa? Nina shida gani? Siwezi kuuvumilia muziki huu na upuuzi huu wote hapa walio nao siku hizi, wanawake hawa wapumbavu wakiimba, ‘Chini, kutoka kwa i—ikulu ya pembe za ndovu,’ ama . . . na haya yote.” Nikasema, “Hapana shaka nina kasoro fulani.”

40 Ndipo Roho Mtakatifu akasema, “Loo, la. Loo, la. Ukiipenda dunia au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.”

41 Kwa hiyo nikawazia, “Vema, sitaki kujirekebisha na ulimwengu huu basi. Hiyo ni kweli.”

42 Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kunifunulia Ujumbe huu. Nisingekuwa na wakati asubuhi ya leo; nilikuwa nimechoka kupita kiasi, mbali na hayo. Labda, Bwana akipenda, asubuhi ya Jumapili ijayo, kama tungali huku. Nina safari za kufanya juma hili. Lakini kama ningali huku asubuhi ya Jumapili ijayo, Mungu akipenda. Ndugu Neville atalitangaza hilo kwenye matangazo yake, Jumamosi. Nasi tutakuwa humu, kujaribu kuuleta Ujumbe huu. Nami nataka kuuleta kwa njia fulani. Ni Ujumbe wa Injili wa siku hizi, saa hii, na msimu huu.

43 Ambao, nimetabiri, miezi sita iliyopita, ya kwamba huu ulikuwa ndio mwaka wa kumalizia kwa Marekani. Nasi tutaona kama ndio, kulingana na Injili, ama sio. Huu ndio wakati ambapo imekwisha. Ama itapanda juu ama kushuka chini, mwaka huu. Hiyo ni kweli.

44 Sasa, ninyi watoto wadogo, ninawatakeni mje na kipande cha karatasi, na myaandike kwenye ukurasa wa kwanza wa Biblia yenu, ili kwamba wakati Ndugu Branham atakapokuwa ameondoka, labda, mtaona kama nilikuwa sahihi ama nilikosea. Mnaona? Nanyi mtajua kama Bwana angali ananena nami, mnaona.

45 Sasa, katika Warumi mlango wa 4, ninataka kusoma se—sehemu ya Neno, kuendelea mbele.

*Basi, tusemeje juu ya Ibrahimu, baba yetu . . . kwa jinsi ya mwili, amepata?*

*Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya matendo yake, analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu.*

*Maana Maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki.*

*Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni.*

*Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki.*

46 Na Bwana aongeze baraka Zake kwenye Neno. Sasa somo dogo, kama wangeliita hivyo, ninalotaka kuwazungumzia, ni *Upendo Wa Kiungu*. Na wakati upendo wa Kiungu umeonyeshwa na kufikia kikomo chake, neema kuu huchukua mahali pake. Mnaona? Sasa mnaweza kuwazia hilo? Sasa litafakarini, ili tulilete karibu sana sasa. Mnaona? Upendo wa Kiungu unapoonyeshwa na kufikia mwisho wake, neema kuu huchukua mahali pake.

47 Sasa ni ja—jambo la kigeni jinsi ambavyo watu, aina ya watu na yale tufanyayo, katika ushirikiano wetu. Sasa, sote hatuna budi kukabiliana na kweli hizi, kwamba kuna watu ambao unapenda tu kuwa karibu nao. Pia kuna watu ambao ni watu wazuri, nawe unawapenda, lakini hata hivyo kuna jambo fulani kumhusu mtu huyo ambalo ni—ni vigumu kwako kuweza kukaa karibu nao. Sasa tunataka kuzungumzia ukweli. Sasa, sababu yake ni kwamba, ni kwa sababu ya mazingira ambayo mtu huyo, mwanamume huyo mwenyewe ama mwanamke, anaumba.

48 Kwa sababu, wewe ni mwumbaji mdogo, kwa kuwa ninyi ni wana na binti za Mungu. Haidhuru uliinama jinsi gani katika dhambi, mngali ni wana na binti za Mungu, kwa sababu umeanguka, ukapotoka, nafsini na niani mwako. Lakini Mungu ndiye Muumba wako. Na katika hali yako ya kuanguka, wewe ni kiumbe kilichopotea, kilichoharibika cha Mungu, kinachotawaliwa na ibilisi, hiyo ni kweli, lakini mngali ni wana na binti za Mungu. “Hataki yeyote wenu apotee, bali wote waifikie toba.” Mnaona? Naye amefanya kila kitu ki—kinachowezezana kwa . . . Ni Mungu Mwenyewe pekee ndiye angeweza kufanya hivi, kutoa na—nafasi kwa kiumbe Chake, kukubali na kuwa jinsi Yeye anavyotaka uwe, urudi kwenye hali yako sahihi tena. Wala hakuna mtu . . .

49 Sasa hili hapa, na ni kali sana: Lakini hakuna mtu aliye katika akili zao timamu mpaka wamempokea Bwana Yesu. Hilo ni neno lenye kilindi, bali ni kweli. Hakuna mtu aliye na akili timamu, mpaka wamemkubali Kristo Yesu kama Mwokozi wake binafsi. Hilo linasikika la kige- . . . Bali ni Biblia. Bila shaka, hiyo ni kweli. Yeye Ndiye. Na katika utu wako uliombwa . . . Sasa, utakuwa mwendawazimu, kwa ulimwengu, unapofanya hivyo. Kwa sababu, inakubidi kutoka katika mazingira uliyomo, uingie katika mazingira haya mengine. Unapofanya hivyo, Mungu anakuinua moja kwa moja kutoka ulimwenguni, nawe unaishi katika mazingira ya kimbinguni. Unaona? Ndipo basi, kwa ulimwengu, wewe ni kinyume tu na kile huo ulicho. Unaona? Na Hii ni kinyume na ulimwengu. Unaona?

50 Sasa yale unayotaka kufanya, ni kuinuliwa juu na Kristo, uingizwe kwe—kwenye mazingira fulani, ambamo una furaha, amani. Halafu, mle ndani, unaumba hali fulani.

51 Na sasa, mara nyingi, sisi katika makanisa . . . Hili linaweza



likaonekana la kigeni, bali mtaliangalia tu. Sasa, hili ni kwa ajili ya kanisa, ni kwa ajili ya watu. Watu hupata roho ya mmoja kwa mwingine, badala ya kumpata Roho Mtakatifu. Ukiingia katika kundi la watu, angalia jinsi mtu huyo afanyavyo. Na—na hao ni watu wazuri wanaokuja katika kusanyiko hilo, muda si muda mnajua, wanatenda vile vile. Sikuzote unaninii . . .

<sup>52</sup> Hebu mchukue mwanamke mzuri na mwanamume mbaya; na ama atajisikia . . . Ama atakuwa mwanamume mzuri, au yeye atakuwa mwanamke mbaya. Basi yale mazingira unayoishia, unaonyesha wenzako jinsi ulivyo.

<sup>53</sup> Basi tunapaswa kuwa watu wa aina gani ikiwa sisi ni Mkristo? Ni mazingira ya namna gani tunayopaswa kuishia? Katika mazingira ya kufariji, kutuliza, kuponya, tunapaswa kuishi ndani yake, huku mioyo yetu sikuzote ikiwa katika maombi, tukiwa na upendo wenye kilindi kwa kila mtu tunayewasiliana naye. Na hiyo iwe ni . . .

<sup>54</sup> Kama nikisema jambo hili, kwa kanisa dogo ambalo limeniombea, kwa ajili ya huduma ya ulimwenguni, huo ndio ufanisi wangu katika kuwaombea wagonjwa. Kama siwezi kuingia ndani kabisa ya hisia za huo ugonjwa pamoja na huyo mtu, kwa kawaida haileti faida yoyote. Inakubidi kushuka chini kabisa mpaka unaninii tu . . . Nawe unauhisi, mwenyewe.

<sup>55</sup> Hapa siku moja, maskini mwanamume Mmeksiko huko chini jukwaani, wakati alipokimbia jukwaani. Imani kuu, alianguka chini, akatoa rosari yake upesi. Ni—nikamwambia, “Haina haja,” na kupitia wa mfasiri, Ndugu Espinoza. Kwa hiyo, akasimama. Akanikumbatia, akaanza kufanya kitu fulani. Alikuwa ni kipofu. Nikamwangalia. Nikaiangalia maskini hiyo miguu iliyojaa makunyanzi, huenda ikawa kamwe hajawahi kuvaa jozi ya viatu, maishani mwake. Nikaviangalia viatu vyangu, nione kama vingemwenea. Ningempa viatu vyangu. Alikuwa ni kipofu. Ndipo nikaangalia, alikuwa mpana zaidi begani mwake. Mtu mkubwa, alikuwa na uzito wa mia mbili na kitu, nadhani. Asingeweza kuvaa koti langu.

<sup>56</sup> Basi wakati alipokuwa amesimama pale, hizo nywele zenye mvi, niliwazia juu ya baba yangu. Nikawazia, “Kama baba angaliishi kufikia yapata umri huu, angalikuwa kama rika moja, mtu kama huyu, yapata umri wa miaka sitini na mitano ama sabini.” Nami nikaingia katika kumpenda mtu huyo, jinsi nilivyowazia. “Labda kamwe hajawahi kula chakula kizuri, maishani mwake. Labda hajawahi kuketi chini mezani, maishani mwake.” Na haya yote, na kisha kutembea katika giza.

<sup>57</sup> Ndipo jambo fulani likaingia moyoni mwangu. Mungu umrehemu! Yeye ni mwanadamu. Yeye ni ndugu. Halafu, Hiyo inapogusa, kuna kitu kinachotia upako. Kuna uumbaji unaojongea karibu, nawe unaninii . . . Unaonyeshwa kwa mtu huyu. Katika dakika chache, nikamsikia akisema jambo fulani

kwa sauti kuu juu ya bega langu. Naye alikuwa akipaza sauti, “Ninaweza kuona. Ninaweza kuona.”

<sup>58</sup> Ilikuwa ni kitu gani? Upendo wa Kiungu. Huruma ilikuwa imeonyeshwa, na Roho Mtakatifu, ndani ya mtu huyu. Na kwa jambo hilo, mwishoni mwa safari, ambapo asingeweza. . . Hakuna kitu kingaliweza kufanywa. Nao upendo ulikuwa umechukua mahali pake, nao upendo ulikuwa umekutana na upendo, ndipo neema kuu ikaanza kutenda kazi. Naye Mungu, kupitia kwa neema kuu, akamrejeshea huyo mtu kuona. Mnaona? Kwanza, huna budi kuingia kwenye wazo hilo.

<sup>59</sup> Hivyo ndivyo inavyokupasa kumfanyia mwenye dhambi. Watu wengi huwaombea wenye dhambi. Hiyo ni sawa. Lakini hiyo siyo njia ya kumvuta mwenye dhambi. Ni kazi yako kumvuta mwenye dhambi. Humvuti kwa kumwomba. Unamvuta, u—unamvuta kwa kuzungumza naye, na kumtambulishia, Kristo. Hiyo ni kazi yako. Huo ndio wajibu wako, ni kuwavuta wenye dhambi kwa kuzungumza nao. Na kuwaonyesha upendo wa Mungu, kupitia kwa Neno la Mungu, linalomvuta mwenye dhambi. Mtu fulani anasema, “Siwezi kwenda kanisani. Hakika ninampenda mwanamke *yule*. Ninampenda jamaa *yule*.” Unaona, kwa sababu unawavuta. Kama ulikaa nyumbani na kumwomba tu huyo mwenye dhambi, kamwe hukuenda kuwasiliana naye, kuna machache sana yanayoweza kufanywa. Lakini inakubidi kuomba kisha uende. Hiyo ni kweli. Nenda ukafanye hivyo. Sasa, kuonyeshwa kwa upendo huu.

<sup>60</sup> Hapa siku chache zilizopita, nilikuwa nikisikiliza ushuhuda wa m—mtengenezaji mkuu wa majembe, akisimama jukwaani. Vema, hapo waliketi wafanyabiashara kutoka kote ulimwenguni, wameketi jukwaani, na mtu huyu wa majembe. Akasimama, akasema, “Vema, sijui ni kwa nini ilinibidi kufanyiwa upasuaji.” Nami ninampenda mtu huyu. Naye ni mfuasi mkuu wa Oral Roberts, rafiki yetu. Na kwa hiyo wakati. . . Yeye akasema, “Nilipogundua kwamba nilikuwa nikiugua na kupata matatizo ya vijiwe, vijiwe vya figo, ilitokea nilikula chakula cha kutwa pamoja na Ndugu Oral.” Basi kasema, “Ndugu Oral alisimama na kusema, ‘Sasa, ndugu, ni—ninaona kwamba unateseka, kwa hiyo,’ akasema, ‘Ni—nitakuombea.’”

<sup>61</sup> “Naye akasema, ‘Vema, Bwana asifiwe! Nilitaka tu wewe useme hivyo, Ndugu Oral.’”

<sup>62</sup> Naye kasema, Oral alimjia na kuweka mikono yake juu ya mafigo yake, “Na kusema, ‘Ninakemea kijiwe hiki cha figo, na kimwache mtu huyu mara moja.’” Kisha kasema, “Wakati alipofanya hivyo,” kasema, “nilipata nafuu.” Ndipo kasema, “Kwa muda mfupi tu, ukarudi tena.” Kasema, “Nikamwendea

tena Ndugu Oral.” Na kasema, “Akaniombea tena. Nikapata nafuu. Lakini, kila wakati uliporudi, ukawa mbaya zaidi.”

<sup>63</sup> Naye akasema, “Halafu, jambo la pili nililowazia, ‘Kama ningeshuka,’” akasema, “kwenda kwa Ndugu Branham, na niweze kusimama mbele zake. Naye Roho Mtakatifu angemjia, angeniambia basi ni kwa nini kwamba sikuponywa wakati Ndugu Oral aliponiombea.”

<sup>64</sup> Kwa hiyo, akafanya safari, akaja Louisiana. Nilikuwa kwenye ibada kule. Nami nikasimama mbele zake, kwa dakika ishirini. Roho Mtakatifu alikuwa kimya, hakusema chochote. Nikamwombea, naye akasema alipata nafuu. Ndipo akashuka akaja, kisha akaenda, akiwa na wasiwasi, amesisimkwa. Akaenda mahali mahali, kila mtu, “Mwombee! Mwombee!” Naye alimpenda Bwana.

<sup>65</sup> Lakini, hatimaye, ikafikia mahali ambapo alikuwa... wakampeleka kwa Mayo. Mayo wakamchunguza, na kusema, “Una nafasi moja kutoka kwa elfu moja, ya kuishi. Imesababisha maambukizi. Mwili wako wote ni sumu, na sumu ya damu,” na, loo, ninasahau mengine yote. Kasema, “Una nafasi moja kutoka kwa elfu moja.”

<sup>66</sup> Kwa hiyo, akasema, “Nikafanyiwa.” Akasema, “Nikaomba, ‘Ee Mungu, unajua ninakupenda. Nami nimewaenda watumishi Wako wote.’”

<sup>67</sup> Naye akachukua fursa hiyo, nao wakampa nusukaputi alale. Naye akasema, wakati alipoamka chumbani, alisema kulikuwa na Nuru iliyokuwa ikiangaza chumbani, nao Utukufu wa Mungu ulikuwa umemzunguka pande zote.

<sup>68</sup> Nao madaktari walishangaa sana. Wangeingia, na kusema, “Vema, ni kitu gani kilichotukia hapa?”

“Mbona,” akasema, “ninajisikia kwenda nyumbani.”

<sup>69</sup> Ilikuwa ni nini? Mnaona, alikuwa amejenga matumaini yake juu ya, “Kama kitu chochote kikiniyata, nitamwendea Ndugu Roberts. Kama hiyo ikishindikana, nitamwendea Ndugu Branham.” Na, hata hivyo, alimpenda Bwana Yesu. Ilimbidi Mungu kuacha mengine yote yashindwe, kumlaza pale kitandani mwake, hata wakati daktari aliposema, “Hatuwezi kufanya lolote.”

<sup>70</sup> Basi wakati upendo wa Kiungu ulipofikia mwisho wake, neema kuu ikaingia ndani na kuchukua mahali pake. Itafanya hivyo kila wakati; kama nia yako ni njema, mibadala yako iko sahihi, kama utakuwa na upendo wa Kiungu, na kuamini, usonge mbele, pasipo kutilia lolote shaka. Inapofikia, kuonekana kana kwamba mwisho wa safari umefika, basi neema kuu inachukua mahali pake.

<sup>71</sup> Jinsi nimeliona likitenda kazi! Jinsi nimeliona katika maisha yangu mwenyewe! Na sio tu kwa theolojia, wala sio kwa namna

fulani ya ujuzi wa m—mtu mwingine. Nina furaha sana, leo hii, kwamba ninaweza kuzungumza kutokana na ujuzi wa kibinafsi, kujua ya kwamba hiyo ni kweli. Kwa nini tunahofu basi? Maadamu tunajua ya kwamba upendo wa Mungu umetulia moyoni mwetu Kiungu, kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, pepo wote kutoka kuzimu hawana nafasi ya kuingia, hata kwenye mauti, kama utaendelea katika upendo huo na imani.

<sup>72</sup> Ni kama tu mtoto mchanga. Hebu mchukue mtoto mchanga... Nitawaonyesha, kusudi jamaa hawa wadogo waweze kulipata. Huyu hapa Bibi Kelly ameketi hapa mbele zetu. Wakati askari mlevi, naamini ndiye, alipowagonga huko nje. Naye akaokotwa, kama maiti, hapa. Walimweka hospitalini, amepoteza fahamu. Wakati kila kitu kilipokuwa kimeshindwa, naye alikuwa akienda zake. Na, bado, akiwa na upendo wa Mungu moyoni mwake, akajirudia. Akaingia mle ndani siku hiyo, ndipo basi neema kuu ikaonyeshwa, baada ya upendo wa Kiungu. Naye huyu hapa ameketi, asubuhi ya leo, miongoni mwetu, yu hai leo hii.

<sup>73</sup> Mnaona, ni jambo fulani ambalo hutukia. Unapofikia mwisho wa safari, unapofikia ambapo huwezi kusonga, ndipo Nguvu za Mungu zitaingia, kwa neema kuu, jambo ambalo unaliona.

<sup>74</sup> Hebu mchukue mtoto mdogo, mtoto mchanga, ambaye ana hamaki, mishtuko ya misuli, nao watapiga mayowe, na kurusha miguu, na kulia. Ndipo muda si muda mwajua, watashikilia pumzi yao. Nawe utamwona mama akimnyakua, na kumvuta, na kumtupa hewani, anampulizia usoni. Achana naye. Kamwe hapajakuwapo, katika historia yote ya matibabu, mmoja ambaye alikufa namna hiyo. Hawatakufa. Yeye ameshikwa tu na hamaki. Anajaribu kupata huruma. Anajaribu kupata uchangamfu, na ni kipindi tu cha hasira. Ndipo baada ya kupata kipindi chake cha hasira, kufikia mahali, ameishikilia pumzi yake, ambapo hawezi kuendelea zaidi, ndipo maumbile yanaingia, anastarehe na kuanza kupumua tena. Kumnyanyua kwako kote, na kupiga mayowe, kunafanya tu... kupiga makelele, na kuupulizia uso wake, kunamfanya mbaya zaidi.

<sup>75</sup> Hivyo ndivyo ilivyo, baada ya sisi kuhama kanisa moja hadi lingine, kwenda huku na huko, kutoka kwenye ibada ya uponyaji hadi ibada ya uponyaji. Ndugu, chukua upendo na usonge mbele, maana uko kwenye mwisho wa safari. Mungu ataonyesha neema kuu unapofikia mwisho wa safari. Wakati upendo umefikia ukamilifu wake, Mungu anawajibika basi. Wakati umefika mwisho wa safari, na mwanadamu amefikia mwisho wake, basi neema inachukua mamlaka. Ni tabia ya Mungu kufanya hivyo.

<sup>76</sup> Jinsi nimeliona! Jinsi ambavyo wakati ningeninii...

Samahani shuhuda hizi za kibinafsi sasa, kwa dakika moja. Mmekisoma kile kitabu. Kutoka huko siku hiyo, huko Portland, Oregon, hapo yule mwendawazimu alipokimbia jukwaani, alikuwa akitaka kuniua. Nyote mmesoma hayo, labda, katika kile kitabu. Ni kitu gani kilichotukia? Mungu alinituma kuhubiri Injili. Ndiyo nilikuwa ninafanya.

<sup>77</sup> Maelfu ya watu walikuwa wamekusanyika. Mitaa ilikuwa imejaa, huku mamia sitini na kitu wakiwa ndani; huku mvua inanyesha, watu wamesimama pale. Mioyo yao ilikuwa na shauku, njaa. Hapo ni wakati hakuna mwingine aliyekuwa hudumani. Madoido yalikuwako mkutanoni. Nao ingewalazimu kukuvuta kupitia kwenye umati, na chochote kile, pamoja na polisi wasindikizaji, kukuingiza ndani.

<sup>78</sup> Nilikuwa nimekuwa chumbani, na hapo nikawaongoza maafisa wawili kwa Kristo, kwenye chumba cha kuvalia nguo; wavulana wawili wadogo, kwenye kikosi cha polisi, kwenye umri wao wa miaka ishirini ya mwanzoni. Mmoja wa mama zao alikuwa ameponywa, usiku uliotangulia. Nao wote wawili wakainama humo, nami nikawaongoza kwa Bwana Yesu.

<sup>79</sup> Kutembea jukwaani, kunena, imani. Mara, mwendawazimu aliyekuwa amempiga mhubiri, huko chini mtaani, alasiri hiyo, aliyekuwa ametoroka hospitalini, aliuvunja mfupa wake wa mtulinga, akavunja shavu lake. Alipenda sana kuwaua wahubiri. Akaingia ndani mbio, nami nikawazia, “Hii ndiyo nafasi yangu.” Akaja moja kwa moja jukwaani, akiwa na uzito wa 250 ama 260, mwenye urefu wa karibu futi sita na inchi kumi, akiipembeza mikono yake mbele na nyuma. Akasema, “Ewe mnafiki! Ewe nyoka nyasini!”

<sup>80</sup> Hilo hapo. Ibada ya Mungu katika utaratibu; watu wakiponywa; maelfu wakiokolewa na kubarikiwa; wahudumu wakivuviwa. Uamsho huu mkuu, kwenye mwanzo wake tu, wakati huo, upate kuanza kuenea kote ulimwenguni. Huko juu, aliketi T. L. Osborn, (Amina!) ambaye ameleta makumi elfu ya watu kwa Kristo; ameketi pale, akilichunga kanisa pamoja na wanane ama kumi katika kusanyiko lake, wakichungulia chini kutoka kwenye roshani.

<sup>81</sup> Naye mwendawazimu huyo akakimbia jukwaani, kuukatiza mkutano wa Bwana. Naye akasema, “Ewe nyoka nyasini! Ewe mnafiki, ukijifanya kama mtumishi wa Mungu. Nitakuonyesha, usiku wa leo, wewe si mtumishi wa Mungu. Nami nitavunja kila mfupa kwenye maskini mwili wako mdogo.” Ndipo akakimbia pale na kuivuta nyuma ngumi yake kubwa, apate kunipiga.

Nikageuka. Wahubiri wakatawanyika, kila kitu.

<sup>82</sup> Kasimama, naye akakohoa, na kunitemea mate usoni mwangu. Akasema, “Ewe nyoka nyasini! Nitakuonyesha wewe ni mtumishi wa Mungu kiasi gani. Ewe mdanganyifu!”

<sup>83</sup> Sikusema hata neno moja. Nilimwalia tu. Ndipo ghafla, Roho Mtakatifu, kitu kingine . . .

<sup>84</sup> Ungewazia nini kama mtu alikutemea mate usoni mwako? Mbona, kama kuna hasira yoyote kwako, ingepanda. Hakika, ingepanda. Basi hapa wakaja polisi wawili, wale wale polisi wawili ambao . . . ? . . . wakiwa na vile vitu mikononi mwao, kumpiga na kumwangusha huyo mtu chini, kumwondosha. Lakini, nisingewaacha wafanye hivyo.

<sup>85</sup> Mungu alikuwa amelea upendo moyoni mwangu kwa mwanadamu huyo. Nikawazia, "Si huyo mtu. Ni ibilisi aliyemwingiza katika hali hiyo. Mtu huyo angekuwa mtu wa kawaida anayetaka kupenda na kuishi, kama watu wengine wafanyavyo. Lakini ibilisi ndiye amemweka katika hali hiyo." Ndipo upendo ukaanza kububujika kutoka ndani, kwa ajili ya mtu huyo. Na muda si muda mwajua, mtu huyo akaanguka kuikingama miguu yangu pale. Wakati upendo wa Kiungu ulipoonyeshwa, neema kuu iliingia na kupachukua mahali pake. Itafanya hivyo kila wakati.

<sup>86</sup> Hapa si muda mrefu uliopita, wakati . . . Huenda niliwaambia haya hapo kabla. Mwaka jana, mwaka uliotangulia mwaka jana, ndivyo ilivyo sasa. Nilikuwa nikikata nyasi kwenye kitalu changu kule juu, nikijaribu kukata nyasi kitalu changu, kote, kote. Ilinibidi kusimama na kubadilisha nguo, nikaingia ndani nikamwombea mtu fulani, nikatoka. Vema, kitalu changu kilikuwa na nyasi ndefu. Kabla mimi . . . Upande wa nyuma, kabla sijazikata za upande wa mbele, zingekua.

<sup>87</sup> Na kwa hiyo mimi, siku moja, nilikuwa upande wa nyuma pamoja na maskini mtambo wangu wa kuzikatia, nikiendelea kuzikata, nikiendelea, nikiijaribu mashine ndogo ya kukata nyasi. Nami nikasahau ya kwamba kulikuwako na kiota cha mavu pembeni pale. Basi nikagongesha hiyo mashine ya kukata nyasi pale. Na huko nyuma, nilikuwa nimevua shati langu, sijavaa shati. Nikaupiga ua huo kwa mashine hiyo ya kukata nyasi, huku sijavaa shati. Katika dakika moja, nilikuwa nimefunikwa na mavu. Mnajua hao ni nini, kiota kikubwa cha mavu; wangekuua. Jamaa wakubwa mno wakivuma! Loo, nikawazia . . .

<sup>88</sup> Kwanza, iliniogopesha. Halafu, mara, jambo fulani likaanza kutukia, nikaanza kutulia. Hao mavu, wangali wanavuma kote. Sasa, hili linasikika kama mtoto, hili linasikika la kitoto. Lakini, Mungu wa Mbinguni anajua kama ni kweli, ama si kweli, Yule ninayemsimamia. Halafu, badala ya kujaribu kupigana, na kuwapiga na kuwaponda hao mavu, kulikuwako na namna fulani ya upendo wa kiungu ulionijia.

<sup>89</sup> Nikawazia, "Maskini jamaa wadogo, mna haki ya kutengeneza kiota. Hiyo ndiyo njia Mungu aliyowafanyia ya kujihami. Nami niliwasumbua, basi kunradhi kwamba nilifanya

hivyo. Kama ingalinibidi kufanya hivyo tena, nisingewasumbua. Sikumaanisha kufanya hivyo.” Lakini, nikasema, “Mimi ni mtumishi wa Bwana. Nao watoto Wake wagonjwa wako hapa kuombewa, nami sina budi kuharakisha na kukatia nyasi kitalu hiki. Sasa, enyi viumbe wadogo wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, rudini kiotani mwenu. Sitawasumbua.”

<sup>90</sup> Basi ilikuwa ni kitu gani? Palikuwa ni mahali ambapo ningaliumwa hata nife. Katika upendo wa Mungu, kwa moyo uliojitolea, kuonyesha upendo kulitokea, ndipo neema kuu ikachukua mamlaka; ambayo ingeweza kuwaambia hao mavu, kuwazungumzia, na kila—na kila mavu akachukua duara yake katika kuruka, na kupanga mstari kama kundi la askari wa kijeshi, nao wakaenda moja kwa moja wakaingia katika kiota chao.

<sup>91</sup> Ilikuwa ni kitu gani? Nisingeweza kuzungumza na hao mavu. Sina njia ya kuzungumza nao. Ningewezaje kuwafanya wasiniume? Nilikuwa mwisho. Bali nilikuwa na upendo. Mungu alitoa upendo kwa ajili ya hao mavu, nami nikazungumza nao kwa sauti yangu. Naye Roho Mtakatifu, kupitia kwa neema kuu, akawaongoza hao mavu moja kwa moja wakarudi kwenye kiota chao.

<sup>92</sup> Si mbali sana chini huko barabarani, maskini Guernsey huko Henryville, siku moja. Huyu fahali mkubwa huko nje, aliyemwua mtu huyu mweusi, kwenye shamba la Brooks huko nje. Alimwua mtu mweusi, karibu amwue mvulana yule wa West, vivyo hivyo. Walimtupa huko nje shambani. Sikujua. Nilikuwa nikifanya doria. Nilipaswa kubeba bunduki; sikuwa nayo.

<sup>93</sup> Siku moja, nikivuka, niliwazia ningeenda—ningeenda kule, kumwomba mtu mgonjwa. Nikaenda kupitia humo shambani, bila kuwazia juu ya fahali huyo kuwa kwenye shambo hilo. Nami nikafikia huko mbali katikati ya hilo shamba. Ilikuwaje? Muda si muda mwajua, kutoka kwenye mafungu hayo ya vichaka, fahali huyu mkubwa mpiganaji akasimama, pembe ndefu *hivyo*, naye akatoa mngurumo. Nikajua huyo alikuwa yule mwuaji.

<sup>94</sup> Nikaangalia nyuma. Nilikuwa mbali sana na ua, yapata yadi mia mbili. Hakuwa amesimama futi thelathini, arobaini kutoka kwangu. Huyu hapo amesimama, amezinamisha pembe zake, akatoa mlio mkubwa. Sikuwa na bunduki, wala mti wa kuufikia. Nisingeweza kurudi uani. Nikawazia, “Vema, huu ndio mwisho. Bill Branham, hapa ndipo utakutana na maangamizi yako, kuuliwa, kupigwa pembe hata ufe, huku nje shambani.” Nikasimama pale.

<sup>95</sup> Lakini, mara, Kitu fulani kikaanza kutulia pale...?... moyo. Utukufu wa Mungu. Kitu fulani kikaingia moyoni mwangu. Nikawazia, “Nilimsumbua maskini mnyama huyo. Si maskini mnyama huyo. Ni ibilisi ambaye anamfanya afanye hivyo.”

<sup>96</sup> Nami ninajua tu jambo moja... Hili hapa. Ninawatakeni mlisikie. Kuna kitu kimoja tu kinachomshinda ibilisi, hicho ni upendo safi wa Kiungu. Upendo utashinda kila kitu. "Mungu aliupenda sana ulimwengu," ukalishinda swali la dhambi, ukalishinda swali la magonjwa. Utashinda tofauti kanisani. Utashinda kila kitu kilichopo kisichofanana Nao, kushindwa. Utashinda, iwapo utauruhusu tu kushinda.

<sup>97</sup> Ndipo wakati mnyama huyu mkubwa alipoanza kunijia mbio. Basi, badala ya kumchukia mnyama huyo, Ndugu Mike, nilimpenda. Nikawazia, "Wewe ni kiumbe cha Mungu. Ni nani mwingine angeweza kukuumba ila Mungu? Nawe ulikuwa umelala pale kwa amani, nami nikapitia kwenye eneo lako, huku kukiwa na matangazo kote shambani. Kamwe sikuyawazia hayo. Niliacha tu eneo langu la kawaida, nipate kwenda kule kumwomba mtu mgonjwa."

<sup>98</sup> Na hapo nikamwona jamaa huyo akija, kichwa chake kikiyumbayumba namna *hiyo*. Naye alikuwa akinijia, kunuia, nami nilijua hivyo.

<sup>99</sup> Lakini upendo wa Kiungu ukaanza kuja. Nikawazia, "Maskini kiumbe, mnyama bubu, hajui vema zaidi. Wewe hapo ulilala, nami nikakukatiza. Kwa hiyo, sasa, mimi ni mtumishi wa Mungu; wewe ni kiumbe cha Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, rudi ukalale chini, kwa kuwa niko njiani kwenda kumwomba mmoja wa watoto wagonjwa wa Mungu. Rudi ukalale."

<sup>100</sup> Ndipo fahali huyo akanikimbilia mbio alivyoweza. Hamna hofu; sikuhofu zaidi ya vile ningemhofu Ndugu Neville anayeketi papa hapa. Upendo safi tu mtakatifu, moyoni mwangu! Ulifanya nini? Uliumba mazingira. Naye fahali huyo akakimbia akaingia moja kwa moja kwenye mazingira hayo. Si zaidi ya futi kumi kutoka kwangu, akasimama na kuitupa miguu yake nje. Akaangalia papa *hapa*, ameshindwa kabisa, akiwa na mtazamo mpole sana usoni mwake, kisha akageuka, akaenda na kulala chini. Nami nikapitia umbali wa kama futi tano. Ni kitu gani? Wakati upendo wa Kiungu unapoonyeshwa, neema kuu huchukua mamlaka wakati huo.

<sup>101</sup> Huyo alikuwa ni Mungu yeye yule ambaye angeweza kuwakomesha simba wasimjie Danieli. Nao walikuja na mngurumo. Naye maskini Danieli amesimama pale, amefunikwa na upendo wa Mungu. Hao simba walimwendea wakalala chini. Kulikuwa kutulivu.

<sup>102</sup> Nakwambia, ndugu yangu, wakati Mungu anapoweza kukufunika katika upendo wa Kiungu, kuna amani bondeni kwa ajili yako basi. Haya basi.

<sup>103</sup> Hapa siku moja, nilikuwa nikija kutoka Dallas, Texas. Nilikuwa nikiruka kwa ndege, nikija nyumbani. Tulikuwa tumekuwa na mkutano kule. Basi nikiwa njiani mwangu, nikaingia kwenye dhoruba, nayo ndege ikalazimishwa kutua



huko Memphis. Basi nilipokuwa Memphis, waliniweka kule kwenye ile Peabody Hotel, loo, mahali pazuri sana pa kujivunia. Kidogo nilijisikia siko mahali pangu. Nilikuwa huko juu usiku huo, nami nikakaa usiku kucha. Wakanipigia simu kesho yake asubuhi na kusema, “Kasisi Branham?”

“Naam.”

<sup>104</sup> Kasema, “Gari la kifahari litakuchukua sasa kwenye saa moja kamili. Ndege itaondoka saa moja na nusu.”

<sup>105</sup> Nikasema, “Asante, bwana,” nikakata simu. Nikaamka, nikaomba. Nami nikawazia, “Vema, ninao wakati, labda, kukimbia kwenye sanduku la posta. Nina barua hapa, nilizozijibu jana usiku.” Nikaamka na kuanza kushuka mtaani, nikishuka mtaani nikiimba:

Wapo watu karibu kila mahali,  
Ambao mioyo yao inawaka moto  
Kwa Moto ulioshuka Pentekoste,  
Uliowasafisha na kuwafanya safi;  
Loo, unawaka sasa moyoni mwangu,  
Loo, utukufu kwa Jina Lake!  
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema  
mimi ni mmoja wao.

<sup>106</sup> Nikishuka mtaani, nikiwa na lundo hili la barua mkononi mwangu, nikielekea posta. Nikahisi Kitu cha kigeni. Mnajua ninayozungumzia, sivyo? Kana kwamba kila kitu kimetulia. Loo, hisia ya jinsi gani! Nikawazia, “Loo, jamani, si ajabu hii!” Sasa, Doc alizoea kuimba wimbo mdogo:

Jalia nitembe na Hua wa Mbinguni;  
Yajaze mapito yangu kwa upendo.

<sup>107</sup> Nilikuwa nikiwazia hilo. Ndipo upendo huu ukaanza kumiminika chini, wa ziada. Tunao upendo, bali tunahitaji wingi wa upendo, upendo unaofurika.

<sup>108</sup> Unasema, “Loo, nawapenda wenye dhambi.” Lakini, loo, ndugu, dada, unawapenda vya kutosha kutoka uende ukazungumze nao na kuwavuta kwa Kristo? Unaona ninalomaanisha?

Unasema, “Ninampenda Bwana.”

<sup>109</sup> Lakini unaweza kumtumainia wakati daktari anapokitikisa kichwa chake? Unaweza kumtumaini wakati kila kitu kingine kimekwisha? Unahitaji ubatizo wa upendo unaofurika, upendo wa Kiungu. Hapo inapoonekana kana kwamba, unapomba, nayo maombi yako hayajibiwi, ungali unampenda? Kuna Kitu kinachoendelea kukutakasa? Hicho ni neema kuu ya Mungu, inabidi ichukue mamlaka. Haina budi kufanya hivyo. Ni tabia ya Mungu. Mungu hawezi kufanya lolote lingine ila kufanya hivyo.

<sup>110</sup> Wakati Mungu alipoiona dhambi ya ulimwengu huu, na kuona kwamba watu walikuwa wakifa, pasipo matumaini,

wala wasingeweza kuokolewa, na hata hivyo alijua ya kwamba watu wangempenda, i—ilimshinikiza Mungu, na ikaithibitisha tabia Yake. Tabia ya Mungu ni upendo. Mungu ni upendo. Nayo iliishinikiza tabia ya Mungu, hata ikambidi kufanya njia ya kuepukia kwa ajili ya wale waliotaka kuepuka. Ndipo akamtuma Mwanawe ulimwenguni, aliyefanywa kwa mfano wa mwili wenye dhambi, kuzipeleka dhambi zetu na magonjwa yetu Kalvari. Mungu alifanya hivyo. Upendo wa Mungu, ukitoka nje, ulihitaji neema kuu.

<sup>111</sup> Wala Mungu kamwe hakusema, “Kama utalifanya; kama utafanya *hivi*, nitafanya *hivi*.” Mungu, pasipo na masharti yoyote, Yeye alimtuma Mwanawe afe mahali pako, na kulitatua swali la dhambi. Haikuwa na uhusiano wowote na yale unayowazia kulihusu, Mungu alifanya hivyo, kwa vyovyote vile. Amina. Upendo wa Kiungu, ukivutwa sana, neema kuu haina budi kupachukua mahali pake. Hamna lingine, wakati upendo wa Kiungu unapowekwa mahali pake sahihi.

<sup>112</sup> Sikilizeni kwa makini. Asubuhi hiyo nilipotoka kwenye hiyo ndege, ama nilipotoka hotelini, nikaanza kutembea mtaani, nilikuwa nikitembea, nikiimba. Mara ghafla, Kitu fulani kikaonekana kumwagiliwa juu yangu, mbubujiko mkubwa wa upendo. Nikawazia, “Loo, laiti ningaliweza tu...Loo, ninaamini, kana kwamba najisikia, laiti ningalimwona mtu wa kumwomba!” Hivyo ndivyo unavyojisikia, wakati kukiwapa na kitu moyoni mwako, kinachovuta.

<sup>113</sup> Hivi majuzi...Naweza kusimama kwa muda kidogo tu tena? Hivi majuzi, mtoto Sara alikuwa mgonjwa. Tulipoanza kuondoka, loo, kulikuwa na joto sana. Nami nilikuwa macho kila usiku, nikipata yapata saa mbili za usingizi, wajumbe kutoka sehemu zote mbalimbali za ulimwengu, inanibidi kukutana na *huyu*, *yule*, kuomba, kuhubiri mara tatu kwa siku. Loo, ilichosha sana! Nilikuwa tu nikienda...Halafu nikatoka nje, na ilinibidi kungojea. Kisha nikaendesha gari maili chache nje ya mji. Nami nilikuwa na usingizi sana, hata mapema asubuhi, hata ikanilazimu kujilaza chini, kando ya barabara, na kulala usingizi. Kidogo, dakika chache, nikaamka na kuanza tena. Kamwe nisingeweza kuendelea kuyafungua macho yangu, nikijaribu kusonga mbele kwa shida, kumfikia mwanamke huyu. Nikivuka hilo jangwa lenye joto sana la Nebraska, nikipitia mle.

<sup>114</sup> Ndipo nikawaza, “Loo, jamani!” Mtoto Sara akipumua tu kwa shida na kutapika. Maskini mtoto huyo alikuwa mgonjwa, usiku kucha. Kesho yake asubuhi, alikuwa mgonjwa sana, ilitubidi tu tulisimamishe gari. Angekuwa mweupe usoni mwake. Halafu, basi, nilikuwa nimechoka sana na kudhoofika, nikawazia, “Ee Mungu! Loo, hali ya mambo ni mbaya sana. Mungu, angalia hapa, si—siwezi kuendesha gari; nimechoka sana. Nami nimekuwa huko nje pamoja na watu Wako,

nikijaribu kufanya vizuri nilivyoweza, naye mtoto Sara ni mgonjwa sana.” Vema, tukaenda. . .

<sup>115</sup> Ndipo nikaenda pale na kuweka mkono wangu juu yake. Nikasema, “Mpendwa Baba wa Mbinguni, Wewe ulinipa mtoto huyu; huyu ni Wako. Nilimlea tu.” Nikaweka mkono wangu juu yake. Kitu fulani kikaanza kujongea moyoni mwangu. Hicho kikakomesha kutapika. Kamwe hakutapika tena, tangu siku hiyo hadi wa leo.

<sup>116</sup> Kesho yake, Becky akaanza, mgonjwa kwelikweli, kama virusi, naye akatapika, maskini mtoto huyo alitapika usiku kucha. Kesho yake, Meda akasema, “Tutanunua Pepto-Bismol.” Akatia vijiko kadhaa na kumpa. Maskini mtoto huyo akaitapika yote.

<sup>117</sup> Tukaingia katika Tetoni. Tulipotoka nchi ya joto, tulianza kupanda juu, alitaka kuiona ile milima ya kupendeza. Asingeweza kufanya hivyo; alikuwa mgonjwa sana. Nikasema, “Mpenzi, angalia hapa. Ninataka kuchukua. . .” Kasema, “Baba anataka kukupiga picha, ili uweze kuuona ule mlima pale.”

<sup>118</sup> Akasema, “Loo, baba, ninajisikia tu kama nakufa.” Na kwa hiyo tukampa Pepto-Bismol nyingine.

Tukaomba, asubuhi hiyo, tukasema, “Bwana, uturehemu.”

<sup>119</sup> Na—na, loo, hilo halikufaa kitu. Kwa hiyo, nikapanda kule juu, nami nikamtoa. Nikasema, “Kipenzi, toka uende kwenye hewa safi.” Kuna baridi. Alikuwa amevaa maskini jaketi yake. Theluji ikiwa juu ya ardhi. Kwa hiyo nikatoka, naye alikuwa akijaribu kuninii. . . Akasema, “Naam, baba.” Anafanya, “uhum, uhum.” Nayo maji yalikuwa yakitoka kutoka kwenye maskini kinywa chake. Nikaangalia, nayo macho yake madogo yamerudi nyuma. Na maskini kinywa chake, kikijaa maji tu kilivyoweza kuwa.

<sup>120</sup> Nikaenda kule. Nikaangalia milimani. Nikasema, “Ninaangalia vilimani unakotoka msaada wangu. Msaada wangu hutoka kwa Bwana.”

<sup>121</sup> Mara ghafla, Kitu fulani kikaanza kupinduka, chini ndani yangu. Loo, laiti ningalikuwa nacho wakati wote. Nikaenda pale kando ya gari, nikafungua mlango. Nikasema, “Angalia hapa kwa baba, kipenzi.” Loo, jamani! Hiyo ilikomesha kule kutapika milele. Dakika tano tangu hapo, naye alikuwa akikimbia kila mahali, akicheza na Sarah.

<sup>122</sup> Ni kitu gani? Upendo wa Kiungu unaponyeshwa, neema kuu inachukua mahali pake. Haina budi kupachukua.

<sup>123</sup> Chini mtaani asubuhi hiyo, nikitembea huko Memphis; turudi kwenye hadithi yangu. Nilikuwa nikishuka humo mtaani, huko Memphis, nikimwambia Bwana, ndipo mara, Kitu fulani kikasema, “Simama.” Nikasimama. Mara, ikasema, “Geuka ukapitie ile njia nyingine.” Vema, hiyo ilikuwa ni kuelekea mtoni.

<sup>124</sup> Nikawazia, “Loo, jamani.” Nikatembea mbele kidogo. Nikawazia, “Vema, hilo lilikuwa tu ni jambo fulani nililoninii tu. . .” Mwajua, unapata wazo, unajua, mara nyingi. Na, mara nyingi, watu hukosea kwa kufuata dhana badala ya uongozi wa Kiungu. Kwa hiyo nikaanza kwenda, nikawazia, “Huko ni kuhisi kwangu tu.” Na, loo, kadiri nilivyoenda mbali, ndivyo ilivyozidi kuwa mbaya. Nikasimama, juu mahali padogo, nikaangalia kila mahali. Kulikuwako na vitu vya kuvulia samaki pale. Nikawazia ningejifanya kana kwamba (watu wakipitia pale) ninaangalia tu vitu hivi vya kuvulia samaki. Nilipofika, kila mtu kwa namna fulani alikuwa ameondoka njiani, kundi hilo, kutoka mahali taa zilipozimwa. Nikasema, “Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, ulikuwa ukitaka nifanye nini? Huyo alikuwa ni Wewe ukitenda kazi moyoni mwangu? Ninajisikia tu kana kwamba ninapasuka humu ndani, Kitu fulani tu kikibubujika.”

Kitu fulani kikasema, “Geuka urudi nyuma.”

Nikasema, “Niende wapi?”

<sup>125</sup> Kasema, “Geuka urudi nyuma.” Haileti tofauti yoyote ni wapi. Endelea tu kwenda!

<sup>126</sup> Nikageuka na kuanza kurudi nyuma chini mtaani. Nikatembea. Nikaangalia saa yangu, ingali inanikusumiza, wakati umepita. Nikaenda mbele kidogo, wakati umepita, saa moja na nusu imepita; kwenye saa mbili, “Loo, jamani, jamani, jamani!” Tayari nilikuwa nimefikia kule chini ambako kidogo ni kama tu nyumba za watu weusi, nyumba nyingi za zamani za weusi huko chini, chini kabisa. Nami nilikuwa nikitembea kule, jua liko huko juu sana wakati huo, mwanzoni mwa msimu wa kuchipusha, mawingu yote yametoweka. Nikawazia, “Vema, niliachwa na ninii yangu. . . Ni—niliachwa na ndege yangu.” Lakini, nikawazia, “Loo, Mungu, mimi. . . Ni sawa kama nikiachwa na ndege, maadamu Wewe. . . Unaniongoza wapi, Bwana? Sijui unakonipeleka. Ninaenda wapi?” Si kazi yangu; endelea tu kutembea. Nikaendelea tu kutembea.

<sup>127</sup> Baada ya kitambo kidogo, nikaangalia. Akiegemea nje langoni, namna *hii*, hapo alikuwa mfano kamili wa maskini shangazi Jemima ameegemea kwenye lango, na mashavu yake manene; amesimama pale, huku amejizungushia shati kichwani mwake namna *hii*, na kufungwa upande wa nyuma. Nilikuwa nikitembea namna hiyo. Ndipo nikamfikia, machozi yakitiririka kwenye mashavu yake makubwa manene namna hiyo. Akaniangalia, kasema, “Habari za asubuhi, kasisi.”

Nikasema, “Mama,” kasema, “njema.”

<sup>128</sup> Kidogo alitabasamu na kuniangalia, machozi machoni mwake. Nikawazia, “Aliniita, ‘Ati kasisi.’” Hivyo ndivyo wanavyomwita mhubiri huko Kusini, mwajua.

Nami nikasema, “Ulijuaje nilikuwa kasisi?”

Akasema, “Nilijua ulikuwa unakuja.”

“Ati nini?”

Kasema, “Nilijua ulikuwa unakuja.”

Nikasema, “Sielewi, Shangazi. Waweza kuniambia?”

129 Akasema, “Unajua, uliwahi kusoma ile hadithi kuhusu yule mwanamke Mshunami ambaye hakuwa na watoto wowote, naye akamwomba Bwana ampe mtoto?” Kisha kasema, “Naye Eliya akaja na kumbariki, naye akamzaa mtoto?”

Nikasema, “Naam, mama. Ninaikumbuka hiyo.”

130 Akasema, “Mimi ni mwanamke wa namna hiyo.” Kasema, “Sikupata watoto wowote. Ndipo nikamwomba Bwana, nami nikamwambia Bwana; kama angenibariki na kunipa mtoto, basi ningemlea kwa ajili Yake.” Kisha kasema, “Yeye akanipa mtoto.” Kisha kasema, “Nimefua nguo kwenye ubao wa kufulia,” maskini makao madogo pale kando. Kasema, “Nimefua nguo ubaoni nipate kumlea mtoto huyu.” Kisha akasema, “Alipokuwa mtu mzima, kasisi, a—alichukua njia mbaya.” Kisha kasema, “Alitoka nje na kundi baya, naye amelala humu, akifa.”

131 Kisha kasema, “Daktari alikuwa hapa, majuzi, wakati alipopoteza fahamu, naye akasema wasingeweza kamwe kumfanyia jambo lolote zaidi. Walikuwa wamempa sita-kwasita Salvarsani, na chochote kile, zebaki, na penisilini; bure. Zinaa, kaswende, wanafikiri vali imetoka moyoni mwake.”

132 Kisha kasema, “Hakuna kitu anachoweza kufanyiwa.” Ndipo akasema, “Alikuwa amelala hapa akifa. Na akasema, ‘Ee Bwana, sitaki kumwona mtoto wangu mchanga akifa namna hiyo.’” Tena kasema, “Mimi—mimi... Laiti ningalimsikia tu akisema ameokoka.” Kisha kasema, “Niliomba, na nikaomba, siku mbili usiku.”

133 Kasema, “Alfajiri ya leo, yapata saa tisa,” kasema, “Bwana alinitia usingizi, nikiwa nimepiga magoti.” Kasema, “Nikaota ndoto.” Kasema, “Niliona mtu akija amevaa suti angavu, amevaa maskini kofia nusu ya kimagharibi imewekwa kando ya kichwa chake. Nikasema, ‘Bwana, mimi nilikuwa mwanamke huyo, lakini yuko wapi Eliya Wako?’ Kasema, ‘Huyu hapa anakuja.’”

134 Kasema, “Nikatoka moja kwa moja kwenye kitanda hicho, nami nimekuwa nikisimama papa hapa tangu wakati huo, nikikungojea.” Hivyo ndivyo nilivyokuwa nimevalia, hasa kabisa.

135 Loo, ndugu, wakati upendo wa Kiungu unapoonyeshwa, mama huyo pamoja na mtoto wake, naam, ratili mia moja na themanini, lakini alikuwa angali ni mtoto wake mchanga, amelala pale, akifa kwa aibu. Haidhuru jinsi alivyokuwa ameleta aibu, alikuwa ni mtoto wake mchanga. Yeye alimpenda. Huo ni upendo wa mama. Haidhuru alikuwa ameleta aibu kiasi gani, angali alimpenda.

<sup>136</sup> Na iwapo huwezi kumsahau mtoto wako mchanga, haijalishi ni nini, basi ni zaidi sana vipi Mungu hawezi kukusahau? Yeye alisema, “Majina yenu yameandikwa kwenye vitanga vya mkono Wangu. Mama anaweza kumsahau mtoto wake wa kunyonya, bali kamwe sitakusahau.” Haidhuru umefanya nini, umerudi nyuma kiasi gani, ni kiasi gani umezama ndani, Mungu angali anakupenda. Mungu anakupenda. Dumisha upendo huo. Usiache ushindwe.

<sup>137</sup> Kwa hiyo, akahema. Akasema, “Loo, kamwe nisingeweza kufanya hivyo.” Naye akasema, “Kasisi, niliota ndoto, nami nikakuona ukija.” Kisha kasema, “Nilipoangalia chini barabarani, na kuona maskini hiyo suti angavu, na hiyo kofia ndogo imewekwa kando ya kichwa chako,” kasema, “Roho akaniambia, ‘Yule pale.’” Ndipo kasema, “Waweza kuingia ndani?”

<sup>138</sup> Nikawazia, “Ee Mungu,” nikawazia, “labda huku ndiko ulikoniongoza, hii ndiyo sababu nilipaswa kuja.” Sikujua.

<sup>139</sup> Nikafungua hilo lango. Lilikuwa na mnyororo na ncha ya jembe juu yake. Sijui kama mmeona moja, ama la. Nikafungua maskini huo mlangoni wa zamani nikaingia.

<sup>140</sup> Ndugu, nimekuwa katika ikulu za wafalme. Nimekuwa katika makazi tajiri sana yaliyopo ulimwenguni. Nimekuwa kwa baadhi ya mamilionea, wenye thamani ya ishirini. . . kufikia dola milioni ishirini na nane. Nimetembea juu ya mazulia yao, huku yameshonwa na uzi wa mahameli, kutoka upande mmoja hadi mwingine, ambapo ningeweza kujilaza chini na kulala kwa urahisi kwenye zulia tupu, wakati hayo ni makazi ya kupendeza.

<sup>141</sup> Lakini hata hapakuwapo na zulia sakafuni. Na maskini kitanda kidogo cha chuma kimewekwa pale; blanketi ndogo ya kawaida imemfunika mvulana huyu. Kulikuwa na bango mlangoni, “Mungu ibariki nyumba yetu.” Nilijua nilikuwa ndani ya nyumba ya Mkristo. Nilijua nilikuwa mahali ambapo maombi yalifanywa. Hamna picha zilizobandikwa ukutani, hamna picha chafu; ila Biblia iliyofunguliwa juu ya meza ndogo iliyo na marmar upande wa juu, imewekwa pale.

<sup>142</sup> Na mvulana mkubwa amelala pale kitandani, vibandiko mkononi mwake, akifanya, “Uhum! Uhum!”

<sup>143</sup> Nikawazia, “Loo, jamani.” Nikaigusa miguu yake; ilikuwa inanata na ni baridi. Mauti yalikuwa juu ya mvulana huyo.

Naye aliendelea kusema, “Loo, kuna giza sana! Kuna giza sana!”

Nami nikasema, “Ati anasema nini?”

<sup>144</sup> Akasema, “Kasisi,” kasema, “amekuwa akiwazia kwa siku nyingi sasa, ya kwamba yuko huko kwenye bahari kuu, amepotea.” Kasema, “Hajui aendako.” Kisha kasema, “Hilo ndilo linaloumiza moyo wangu.” Kasema, “Anaondoka, naye

amepotea, huko nje baharini, wala hajui anakoenda.” Kasema, “Kasisi, nimeomba. Nimefanya kila kitu. Nimefanya kila kitu. Sitaki apotee, kasisi.” Kisha kasema, “Hiyo ndiyo sababu nilikuwa ninaomba.”

Nikasema, “Shangazi, mvulana huyu ana shida gani?”

145 Akasema, “Ni ugonjwa wa zinaa. Mtu daktari tayari amesema yuafa, hakuna cha zaidi anachoweza kufanyiwa.” Kisha kasema, “Amepoteza fahamu. Amepotea baharini siku mbili.”

Kasema, “Waweza kumwombea?”

146 Nikasema, “Shangazi, jina langu ni Branham. Ulipata kusikia habari zangu?”

Akasema, “La, bwana. Siamini nilipata kukusikia, kasisi.”

147 Nikasema, “Vema, nitakwambia hadithi.” Nikasema, “Huduma yangu ni kuwaombea wagonjwa.”

Akasema, “Kweli?”

148 Nikasema, “Naam.” Kisha nikasema, nikamwambia kuhusu kutua kwa ile ndege, na kila kitu.

Akasema, “Hiyo ni kweli, kasisi?”

Nikasema, “Naam.”

Akasema, “Vema, nilijua hutanisikitisha.”

Nikasema, “Wewe omba dua, Shangazi.”

149 Naye akapiga magoti pale, nawe nena juu ya maombi! Loo, ndugu, jinsi maskini mtakatifu huyo angeweza kumshika Mungu. Hapo yeye akaomba, mpaka machozi yakatiririka machoni mwake.

Nikaangalia juu. Naye aliendelea kufanya, “Wuu!”

Nami nikasema, “Sasa, Shangazi, nitaomba. Wewe moja kwa moja pamoja nami.”

150 Nikaweka mikono yangu juu ya miguu yake. Nikasema, “Baba wa Mbinguni, ndege yangu tayari imeondoka, nijuavyo mimi. Na hapa maskini mama huyu alikuwa akimlilia mtoto wake mchanga. Na kadri nijuavyo mimi, hapa ndipo uliponiongoza Wewe. Ninaomba ya kwamba utamrehemu.”

151 Na mnamo wakati huo, nikamsikia akisema, “Mami, loo, mami!”

152 Akasimama na kuyapangusa machozi yake kutoka machoni mwake, akasema, “Naam, kipenzi. Mtoto wa mami amepata nafuu?” Akaanza kumpapasapasa kichwani.

153 Akasema, “Mama, chumba kinaingia mwangaza. Chumba kinaingia mwangaza.”

154 Upendo mkuu! Upendo wa Kiungu ulipoonyeshwa kwenye moyo wa Mungu, ilibidi neema kuu ijibie mahali pake.

Ninapowazia, ya kwamba mama maskini pale, akishikilia pamoja na maombi yake kwa Mungu, na yote haya! Basi ilikuwaje? Mungu, kwa neema Yake; Mungu, katika rehema Yake, angeitoa ndege hewani na kuishikilia ardhini, kujibu maombi ya mwanamke mweusi maskini, asiye na elimu, hapo upendo wa Kiungu ulipoonyeshwa. Haijalishi alikuwa ni maskini kiasi gani, jinsi alivyokuwa mweusi, jinsi alivyokuwa wa manjano, kile alichokuwa; neema ya Kiungu inapoonyeshwa, neema kuu haina budi kupachukua mahali pake. Upendo huo wa maskini mama yule pale, jinsi alivyolia!

<sup>155</sup> Naye huyo mvulana, ninii michache...Yapata miaka miwili baada ya hapo, nilishuka kule, nami nilikuwa kwenye garimoshi nikienda huko chini. Nikatoka, nami nakapanda kule kununua hambaga. Walitaka kama senti sabini ama themanini kwake, kwenye ndege, nami...kwenye garimoshi. Nami ningeweza kuinunua kwa yapata senti ishirini kwenye hicho kibanda kidogo. Nikatoka kwenye garimoshi, nikaanza kushuka chini. Kulikuwako na mbeba mizigo, aliyesema, "Aloo, Kasisi Branham!"

Nikaangalia pande zote. Nikasema, "Habari za asubuhi, mwanangu."

"Vema" kasema, "kwani hunijui?"

Nikasema, "La, siamini ninakujua."

<sup>156</sup> Kasema, "Unakumbuka, yapata miaka miwili iliyopita, uliposhuka kuja kuniombea? Pamoja na mama yangu kule?"

Nikasema, "Kwani wewe ndiwe yule mvulana?"

<sup>157</sup> Kasema, "Naam, bwana, Kasisi Branham." Kasema, "Sio kwamba tu nimeponywa, bali nimeokoka sasa. Mie ni Mkristo."

<sup>158</sup> Neema kuu! Naam, bwana, ndugu! Ninawaambia, wakati neema...Wakati Mungu anapooni upendo umeonyeshwa, neema haina budi kupachukua mahali pake.

<sup>159</sup> Majuma machache yaliyopita, nyumbani kwangu, mnaikumbuka; wengi wenu, vema, wakati maskini yule oposamu aliyelala kuingama pale. Wakati, msichana huyu mdogo hapa alipokuwa amemzamisha mtoto wake. Na wakati Mungu alipompa mtoto; wala yeye hakutaka kumlea, basi akamfunika blanketi na kumtupa huko nje na kumzamisha mtoni. Nikasema, "Huyo si mama. Huyo ni duni kuliko mbwa. Mnyama asingefanya hivyo."

<sup>160</sup> Na kama upendo mkuu wa Mungu utaninii, ungeweza kuonyeshwa kwa mnyama, ni zaidi sana jinsi gani ungeweza kuonyeshwa kwa mwanamume au mwanamke? Hiyo ni kweli.

<sup>161</sup> Naye huyu maskini oposamu akipanda kwenye ule ujia, mnaijua hiyo hadithi. Na jinsi alivyoingia, na kulala hapo kwenye vipandio vyangu, saa ishirini na nne, bila mimi hata kujua lolote kuhusu hilo.



162 Ndugu Wood na hao wengine wameketi kule nyuma, na Dada Wood, wakikihurumia kitu hicho, kasema, “Ndugu Branham, kwa nini kumwacha ateseke? Na maskini watoto hao wachanga wa oposamu wakiyanywa hayo maziwa kutoka kwake; yeye amelala hapo, amekufa?” Kasema, “Kwa nini usiwaue, Ndugu Branham, ama umwangamize maskini mama huyo?” Hakuwa amekufa kabisa. Alikuwa... Ungeweza kumgonga, naye... angeweza kujimudu.

Na, hapo, yeye alilala hapo usiku kucha.

163 Ndipo kesho yake, maskini Becky pale, akatoka nje, akasema, “Baba?” Vema, kesho yake asubuhi, yapata mapambazuko, akasema, “Utafanya nini na huyo oposamu, baba?” Kasema, “Nimekuwa nikiwazia tu juu yake usiku kucha.”

164 Nami nikasema, “Nami pia, Becky.” Nikashuka kwenda chumbani. Nikasema, “Rudi ukalale, kipenzi. Ni mapema sana kwako kuamka.”

165 Nikaketi chini mle katika chumba changu cha faragha. Nikawazia, “Vema...?...” Nikawazia, “Itanibidi kufanya jambo fulani na maskini oposamu huyo. Sijui la kufanya.”

166 Ndipo nikasikia Sauti, kwa vile hata sikuwa nikiitarajia.

167 Papo hapo, wakati matofaa yaliposhuka asubuhi hiyo, kwa ajili ya Ndugu Hall, wakati alipoonywa, kansa. Hapo ambapo wagonjwa na wanaoteseka wameponywa. Nilikuwa nimeketi katika maskini kile chumba kidogo, cha faragha.

168 Nikasikia Sauti ikisema, “Nimemtuma kwako. Amekaa kama mama wa heshima, kwa muda wa saa ishirini na nne, akingojea wakati wake wa kuombewa. Wala kamwe hujasema neno Kwangu kumhusu.”

169 Nikasema, “Vema, hata sikujua hilo.” Nikasema, “Vema, unamaanisha ya kwamba Wewe ulimtuma oposamu huyo hapo?”


170 Nikawazia, “Nina shida gani? Kwani ninajizungumzia?” Nikajikuta nikijisemesha mwenyewe.

171 Nikatoka hapo nje, mtoto Becky alikuwa angali anachungulia mlangoni. Nikaenda pale. Maskini yule oposamu pale; huku amefunikwa na umande, na kadhalika. Nikasema, “Baba wa Mbinguni, endapo umemtuma maskini oposamu huyo, asiye na maarifa, kama Wewe umemtuma hapa, kwa njia fulani, mimi... ukaweka moyoni mwangu upendo kwa ajili yake, akiwa mama, hata nisingeweza kumwua, nisingeweza kuwaua watoto wake. Na neema kuu, kuwafundisha hao watu wengine, kwamba inawapasa kujua, umemleta hapa. Basi, Mungu, ninaomba katika Jina la Kristo, ya kwamba utamponya.”

172 Ndipo maskini oposamu huyo, huku miguu yake imejaa funza, na kwa hiyo aliikokota nyuma yake, ikavimba maradufu ya ukubwa wake; akasimama kwa mguu huo. Na kuwaokota hao

watoto, mfukoni mwake, akatembea kupitia pale kwa kawaida tu kama mnyama yeyote alivyopata kutembea. Akageuka, kwangu; kama kugeuka kabisa, kusema, “Asante, bwana mwenye huruma.” Kadiri ni juavyo, wao wana furaha sana pamoja na watoto wake leo hii.

<sup>173</sup> Kwa nini? Upendo wa Kiungu unapoonyeshwa, neema kuu hupachukua mahali pake. Jamani, ndugu, dada, kuna jambo moja tu la kufanya maishani mwako, hilo ni, “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, kwa nguvu zako zote, kwa nia yako yote,” na uamini kila Neno alilosema ni Kweli. Ndipo utakapofikia mwisho wa safari yako, ambapo huwezi kuendelea mbele zaidi, basi neema kuu ya Kiungu, itaonyeshwa.

<sup>174</sup> Ningewezaje kuzungumza naye, akiwa amelala huko, wakati Mayo Brothers walikuwa wamenikatia tamaa, huku nimeketi kando ya lile baraza kule, huku Ndugu Cox ameketi pamoja nami, akishangaa ni kitu gani kilichokuwa kikitendeka. Hata nisingeweza kuvumilia jambo hilo tena. Lakini nikasema . . . 

56-0826 Upendo Wa Kiungu  
Branham Tabernacle  
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)